

6. Kampuni za Biashara za Mikoa (Regional Trading Companies).
7. Vyama vya Ushirika (Co-operative Societies).
8. Uuzaji Bidhaa jumla (Wholesale Trade).
9. Ujenzi wa Kondrasi (Building Contractors, Electrical Contractors, Mechanical Contractors, Civil works Contractors etc.).
10. Utaalam au Ushauri wa Kitaalamu (Specified professionals).
11. Uchapishaji vitabu na Magazeti (Printing and Publishing of Books and Newspapers).
12. Vipuri (Spare parts, machine tools).
13. Udalali (Broker).
14. Usafirishaji wa abiria mijini (Transportation of Passengers within the City, Municipal and Township).
15. Viwanda vidogo (Small Scale Manufacturing and Selling).
16. Simu za kwenye vibanda (Attended Telephone Services).
17. Biashara yoyote ambayo haikutajwa na ambayo haina sura ya kitaifa au kimataifa na isiyoongozwa na sera (any other business which is not of National/International nature or not governed/proceeded by Policy).

MASHARTI YA KUOMBA LESENI ZA BIASHARA KWA MAKUNDI "A" NA "B"
(APPLICATION REQUIREMENTS FOR BUSINESS LICENCE IN SCHEDULE "A" & "B")
 Fomu za maombi ziambatanishwe na (Attach application forms with):-

1. Photocopy ya Certificate of Incorporation au Registration, kama ni jina la biashara. (Attach photocopy of Certificate of incorporation (in case of a Company) or certificate of Registration in case of Business Name and Extract).
2. Kama ni Kampuni, "Memorandum, and Articles of Association" ambazo zitaonyesha kuwa Kampuni imeruhusiwa kufanya biashara anayoiomba (Memorandum and Article of Association showing among other things, that objectives of the company allows it to do the business which is being applied).
3. Uraia: Photocopy ya passport ya Tanzania au cheti cha kuzaliwa au Hati ya kiapo (affidavit) kuonyesha kuwa ni Mtanzania, na kama mgeni alete Hati ya kuishi nchini daraja la "A" (residence permit class "A") inayomruhusu kuwekeza katika biashara hiyo. (Proof of Tanzania citizenship e.g photocopy of passport, birth certificate or in case of non-citizen, Residence Permit Class "A" - showing the holder to be investor in that company/business).
4. Endapo wenye hisa wote wa kampuni wapo nje ya nchi itabidi maombi yaambatane na hati ya kiwakili (powers of attorney). (In case the shareholders of the company are non-residents, Powers of Attorney to a citizen/Resident should be submitted/attached).
5. Alete ushahidi wa maandishi kuwa ana mahali pa kufanyia biashara (Proof by the applicant having a suitable business premises for the business applied, (the following can be submitted as a proof, a copy of title deed, Tenancy agreements, Receipts of Rent or Property payment).
6. Hati ya kujiandikisha kama mlipa Kodi TRA (Tax Payer Identification Number (TIN)).

MASHARTI YANAYOHUSU BIASHARA MAALUM (ADDITIONAL REQUIREMENTS FOR SPECIFIC BUSINESS)

7. Leseni ya Wakala wa Forodha (Customs Agency licences) kwa biashara ya Clearing and forwarding tu. (Customs Agency licence (CAL) for those applying clearing and forwarding licences).
8. Tourism Agency licence (TALA) kwa biashara za, utalii tu mfano mahoteli ya kitalii, Travel Agency (Wakala wa usafiri), Tour operators n.k. (Tourist Agency licence (TALA) - for those applying licences related to tourist promotions e.g. tourists Hotels, Travel Agents, Tour operators, hunting etc.
9. Hati ya utaalam (Professional certificates) - kwa biashara zote za kitaalam - mfano leseni za kuendesha hospitali; zahanati, udaktari, sheria, ujenzi, uhandisi, urubani wa ndege, captain wa meli n.k. (Professional certificates/Authority for all professional businesses e.g. running hospitals, dispensaries; advocates, pilots, ship captains etc.).
10. Hati zinazohusu chombo kufanya kazi ya uchukuzi (Air Worthiness kwa ndege na Sea Worthiness kwa meli) (Certificate to authorize aircraft to fly (Air Worthiness) or ship to sail (Sea Worthiness)).